

# MJI NA UMMA

- **Je, kupenda kwako mji wako yapingana na mafundisho ya dini?**

- **Je, kutilia umuhimu kwako jambo la Waislamu yapingana na kujinasibisha kwako kwa mji wako?**
- **Je, na mji ni kitu tu basi sawa na foko la mchanga katika kiganja chako?**

- **Je, kutilia umuhimu mji wako na kuwa na kite nao ni jambo la kijahilia?**
- **Je, mji ni mambo ya kisiasa tu?**

**Minyororo (Msururu) Wa Kupotesha Na Kuzusha**

Uislamu uko mbali na wenye itikadi kali ambao wanadai kuwa maslaha ya umma yanapingana na maslaha ya nchi.

SW

BARUA NAMBA 11 - MINYORORO NAMBA (116) 2018

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu mrehemevu mno na mwingi wa kurahamu.*

Kila jinsi ya sifa njema yamstahiki Mwenyezi Mungu. Rehma na amani zimwendee bwana wetu Mtume wa Mwenyezi Mungu na juu ya jamaa zake na maswahaba zake na kila mwenye kumfuata yeye.

## Umbile la Mwenyezi Mungu

Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu kwa uzuri wa Qudura zake. Akapatia ndani yake umbile la ubinadamu. Akautia katika umbile hili msingi ya maisha ya hali ya juu na tabia za hali ya juu. Yote hayo ni njia ya kumkirimu yeye na kumtofautisha na asiekua yeye kutokamana na viumbe vingine. Akamuaandalia mwanadamu kwa sababu ya tabia hizo tabia za kimaumbile ili apate kuwa khalifa mbadala au naibu au kiongozi wa Mwenyezi Mungu katika ardhi yake. Jumia ya zenye kuunda hilo umbile au tabia ya mwanadamu huyo -- ikisalimika kutokamana na ufisadi au zenye kuharibu-- ndio jumia ya kujenga dini ya haki. Asema Mola aliyetukuka jambo lake kwa mujibu wa qurani:
{Umbile la Mwenyezi Mungu ambalo kwamba amewaumba nalo watu juu yake hakuna kubadilika kwa umbile lake} [Surah Rum:30]. Kuanzia hapo utaona kuwa ubinadamu hutangulizwa kabla ya dini.

**Mafungamano (usiano) ya kibinadamu katika umbile la Kimola:**

Na katika ambayo Uislamu umetilia nguvu juu yake kutokamana na mambo ya umbile ni kutoa maana halisi ya mafungamano au usiano wa kibinadamu. Twakusudia kuwa hilo mafungamano ya mwanadamu kwa sehemu na zama na watu katika mda wa umri wake katika uhai au maisha ya duniani.

Na hakika ulichora Uislamu kwa ubinadamu kwa mafundisho ya hali ya juu katika jambo la huu usiano (mafungamano) kwa mambo yanayohifadhi kutunza na kutilia nguvu na yanayoweza kunakikisha malengo au makusidio ya hekma ya Mola katika kuviumba kwa namna ya kuwa kwake hali ya kuwa matakwa ya Mwenyezi Mungu katika viumbe vyake ambao si weko au haikuwekwa na mwanadamu.



Akateremsha sheria ambazo zinapanga mafungamano na zinampatia majukumu na yote yanayofungamana juu ya hayo kutokamana na malipo na adhabu.

**Je, mji ni kitu sawia na teko na mchanga katika kitanga chako kama ambavyo wanavyodai?!**

Uwazi wa Maana ya Mji:

Mji ni sehemu ya mwanadamu na matulizo yake. Twakusudia kusema hivyo kuwa ni mashukio ya mwanadamu ambayo ameridhia hali ya kuwa ndio mahala pa kuishi kwake na iwe maisha yake juu ya njia ya kutulia. Huenda ikawa uhakika ni mji wa mwanadamu ni sehemu ya kuzawa kwake na huenda ikawa ni mahala alipoguria na akaishi ndani pake mda kutokamana na zama mpaka pakawa ndio makazi yake na kutambulika kwa hiyo sehemu.
Tena yeye na jamaa na karaba zake na watu na majirani na marafiki na vipenzi vyake na wote kuwa hapo...

Bali huwa mji ni taifa na maendeleo na historia na ukombozi na hukumu kukawa na watu hodari walioweza kuunda historia ya hiyo mji kwa nyanja tofauti tofauti

Na ni mkusanyiko wa hisia au kilicho na ukumbusho ambao kwamba humpitilia mwanadamu kwa kupatikana utendaji na kuamiliana na waliotangulia...

Kwa ajili ya hivyo basi hakika maana au pendeleo la mji ni kusudio la kitu kilichopandamana iliyoshikana. Wala haifai kujikatia yeye kipande chochote au sehemu yoyote na kusemwa kuwa "Ni kitu tu sawia na teko la mchango katika kitanga isikuwa na kima thamani."

Na kujingikiwa au kutojua zote hizi ambazo zinaunda maana au kusudio la mji na kuikatia katika kuwa kitu tu katika katika kusanyiko la mchanga (kwa maana ni kitu kisichokuwa na maana) ni sawa na kukeuka haki ya kibinadamu au umbile alilomuumba yeye nalo na fahamu mbaya au potovu na ni kudharau jambo kubwa au lililo muhimu zaidi. Kwa hivyo kulisemwa:

**"Ukitaka kumjua mtu wa kiislamu, angalia vipi mapenzi na kutamani chake katika miji yake."[1]**

## Fahamu Zilizo Makosa na Bayana Zisizokubalika:

Mawimbi na makundi ya kidini ni yenye misimamo mikali na itikadi kali imekua ikitoa mda mrefu na wala hazijaacha kubabaisha katika kuleta maana isiyokuwa ya "mji na ukazi"!

Na kaleta mazingatio ya kuwa yapingana na upeo wa Uislamu pamoja na umma moja (bi maana malengo). Na hilo ni kwa dhana za ufahamu zao za makosa upande wa dini hii ya haki na kuwa msingi wake wa juu.

Mambo yanayomfanya barobaro wa Kiislamu kuishi hali ya msonga na maisha yake katika mafungamano au uwiano wake pamoja na ardhi ambayo alizawa ndani yake na kukulia ndani yake na kunasibiana kwake... kwa kujihisi kuwa hali yake ya kidini inamfaradhisha (inamlazimisha) yeye kufungamana na kunasibiana na pande la ardhi lote la Kiislamu lilo kubwa na yamzuia yeye kubaki kuvaana na hali ya kimji.

Na hilo ukilijenga juu ya fikia na ufahamu wa makosa limetoa natija ya fikra potofu linaloendelea kusambazwa na kulinganiwa juu yake.

1- Ameipokea Ad-Daynuri katika kitabu "al-Mujalasa wa Jawahir al-Ilm" (No 332) kutoka njia ya al-Asma'i kutoka kwa mbedui.

**Fikra Potofu za Muhalifu na Namna ya Kumregesesha Nayo:**

Kwa watu wenye fikra ya itikadi kali, fikra nyingi juu ya swala la kupenda mji. Miongoni mwayo:

- Hakika kupenda mji haikutajwa katika Sheria wala haikuja ndani yake!
- Hakika ufahamu wa mji yapingana na kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake!
- Hakika ufahamu wa kupenda mji ni fikra za kijinga!
- Hakika mji ni kitutu cha kisiasa chenye malengo ya kuwapiga Waislamu vita!

## Kupenda Mji Kwa Mujibu Wa Quran Na Hadithi Na Kwa Wana Vyuoni Wa Umma

# Quran Yaishiria Katika Kupenda Miji:

Imekuja katika mapekesho mengi kutokamana na dalili ufahamu wa uwiano na kupenda mji na kuwa kafiri mji na katika mambo mazito juu ya nafsi ya mtu. Na ikataja Qurani hilo kwa njia ya kuthibitisha (bi maana uwepo wake katika maisha ya watu) na kukubali, wala haikuja juu ya njia ya kutukanya na kukataza.

Amesema Mwenyezi Mungu: {Na lau kuwa Sisi tumeamrisha wao kuwa jiueni au tokeni majumbani mwenu} [an-Nisa:66]. Ukiangalia utaona imefanywa kufariki mji ni sawia tu na kuua nafsi.[2]

Na amesema Mwenyezi Mungu: {Mwatoe popote walipa, kwani fitna ni mbaya kuliko kuua} [al-Baqara:191]. Amefanya kufariki mji uliyozoea ni balaa kubwa.[3]

2-Angalia at-Tafsir al-kabir ya Imam ar-Razi (15/165).

3-Angalia Mirqat al-Mafatih (Ngazi za Mifunguo) cha Imam Mula Ali Qari (7/582).

## Kutetetea Mji ni Jihadi Katika Njia ya Mwenyezi Mungu:

Amesema Mwenyezi Mungu: {Wakasema itakuaje tusipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na hali tumetolewa majumbani mwetu na watoto wetu} [al-Baqara:246]. Akafanya kutolewa kutoka majumbani (mji) ni miongoni mwa sababu za vita katika njia ya Mwenyezi Mungu. Quraani tukufu imekiri maneno yao na wala haikuwatia aibu juu ya hilo (la kujinasibisha mji).

## Sheria Imefanya Kufariki Mji ni Katika Miongoni mwa Adhabu Kutiwa Adabu kwa Wale Wakosa:

Mwenye ushindi na aliyetukuka akatajia wale wanaoleta vita na mashifta: {Hakika si lengine malipo ya wale wanaompiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wakawania kufanya uchafuzi katika ardhi au nchi ni kuuwawa au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na yao kinyumenyume au kutolewa nchi} [al-Ma`ida:33].

Amesema Imam Shafi'i: Yamtosheleza yeye kafarikishwa mji na jamaa kufedheheshwa na unyonge.

Mwenyezi Mungu aliwaadhibu Wana wa Israeli aliwafanya wametahayari hawajui pa kwenda katika ardhi bila ya makazi, miaka arubaini hali ya kuwaadhibu tu. {Akasema nchi hiyo wameharamishiwa mda wa miaka arubaini watakua wakitangatanga katika ardhi. Basi wawe watu wapotevu} [al-Ma`ida:26].

Basi kufariki mji kwa wenye akili ni jambo zito sana, iliyo sawa uchungu wake na uchungu wa kuua nafsi tu. Nayo ni miongoni mwa adhabu kali kwa nafsi juu yake na kujulisho kuwa kupenda mji na kufungamana nao ni jambo zito katika nafsi.

## Kupenda Mji Katika Sunna ya Mtume:

Amepokea Bukhari katika Sahih yake kuwa Mtume mtukufu wa daraja (rehma na amani ziwe juu yake na jamaa zake) alikuwa akiwa yuatoka katika safari na akaona kuta za Madina, humkimbiza ngamia wake na kufanya haraka kuingia. Na akiwa na mnyama mwengine humharakisha. Yani alikuwa akifanya hivyo kwa sababu ya kupenda kwake Madina. Asema al-Hafidh Ibn Hajar, "Ni kijuiishi au ni dalili juu ya Madina na kule kumewekezwa Sheria ya kupenda mji na kuutamani."[4]

Katika kisa cha mwanzo wa kushuka Quraani juu ya Mtume mtukufu wa daraja (rehma na amani zimshukie yeye na jamaa zake) na kwenda kwake kwa Waraqa bin Naufal na neno la Waraqa kwa Mtume Mtukufu wa daraja (rehma na amani ziwe juu yake na jamaa zake), "Natamani niwe pamoja nawe pindi watakapo kutoa wewe watu wako." Akasema Mtume (rehma na amani ziwe juu yake na jamaa zake), "Je ni wenye kunitoa katika mji?"[5] Asema Suhayli: Huchukuliwa kutoka kwa ufahamu wa maneno hayo uzito wa kufariki mji katika nafsi kwa kuwa Mtume (rehma na amani zimshukie) aliskia kutoka kwa Waraqa kuwa watamuudhi na watamkanusha na wala hakuonyesha kubabaika kwa hilo lakini alipotajiwa yeye la kutolewa ilitaharaki nafsi yake kwa ajili ya kupenda mji wake na vile vile kuzuia kwake kwa mji wake.

## Kupenda Mji kwa Wanavyuoni Wema

Wanavyuoni wana nukuu nyingi na kuthibitisha na kuzingatia juu ya kupenda mji na kufungamana nayo. Yameshatangulia maneno ya Ibn Hajar na as-Suhayli. Bali wameenda wanavyuoni wote kutoa sababu ya msingi ya Hajj ya kuwa na malipo kwa Mola kuwa ni sababu yake nafsi kwa kuifariki mji yake na kutoka kwenye mazoea. Alisema Imam al-Qarafi, "Na maslahi ya (malengo yake) ni kutia adabu nafsi kwa ajili ya kuifariki mji."[6] Na wala haya desturi ya wema katika kupenda mji wao.

4-Sahih al-Bukhari (namba 1802) (Kitabu cha Hijja). Na angalia Fath al-Bari cha ibn Hajar (3621/).

5-Imepokewa na Bukhari na Muslim; Bukhari (namba 3) (Mwanzo wa Wahyi), na Muslim (namba 160) (Kitabu cha Imani), na wasiokua wao wawili kutoka hadithi ya Nana Aisha (radhi ya Mola iwe nae). Na angalia Fath al-Bari cha ibn Hajar (12359/).

6-Angalia al-Dhakhira (Akiba) cha al-Qarafi (3194/).

Mpaka imepokewa kutoka kwa bwana walioipa nyongo dunia na bwana wa wenye kufanya ibada Ibrahim bin Adham kuwa alisema, "Sikuona uzito kitu katika nilivyoiacha ilokua uzito zaidi kwangu kuliko kuifariki mji."[7]

Hajachukua kupenda mji ni jambo lenye kuenea kwa waliotangulia na yakunjuka maudhui ya maneno ndani yake mpaka wakaipwekesha mjungu. Akatunga al-Jahidh kitabu, "Hubb al-Watan." Na akatunga as-Sam'ani "an-Nuzu' ila al-Awtan." Na Abu Hatim as-Sijistani kitabu "as-Shawq ila al-Awtan." Na Abu Hayyan at-Tauhidi kitabu, "al-Hanin ila al-Awtan." Na wengineo wengi kutokamana na waliotunga katika kusudio hili kutoka zamani waliotangulia na wa kisasa.

## Hakuna Upingamizi Kati ya Kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Kumpenda Mji

Kupenda mji ni umbile. Kama vile kupenda mke na watoto na wazee hazipingani na kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake bali vyashikana na yajengeka juu ya kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na vile vile kupenda mji.

Na hutoa hoja hao kwa neno lake atukusho asema: {Ikiwa babazenu na wana wenu na ndugu zenu na wake zenu na jamaa zenu na mali mlioyachuma na biashara mnazoogopa kuharibika na majumba mnayoridhia, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na jihadi katika njia yake basi ngojeni Mpaka mwenyezi Mungu alete amri yake} [at-Tawba:24].

Muhalifu alifanya hii aya ni yenye kutilia nguvu upande wake na kutolea dalili ya kutokana katika kufungamana na mji. Wanasema. "Hakika ya mji ni {majumba mnayoridhia.}"

Ikiwa kwa ufahamu wa kinyume wayo walienga wao na kuwagonga wao. Aya hasa inatilia nguvu juu ya kupenda mji na kufungamana nayo. Ndio twaweza kuwaafiki juu ya kuwa mji ni {majumba mnayoridhia}, lakini twawakhalifu na kukhalifiana nao ni fahamu yao.

7- Hilyatul Awliya (Pambo la Mawalii) cha Abu Nu'aym (7380/) katika tarjama ya Ibrahim bin Ad-ham.

Hakika Mwenyezi Mungu aliyetakasika ametaja mji {majumba mnayoridhia} katika sehemu moja na baba au wazee na watoto kwa namna ya uhakika kuwapenda wao ndio umbile la Mwenyezi Mungu au ndio dini yake. Na akapanga juu ya hilo haki katika sheria. Mwenye kuihifadhi tu ametwii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na mwenye kupoteza haki zao amemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na uhakika wa hapo anaetukanwa ni yule anae hivyo vyote juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Hatakikani yeyote atakae tanguliza juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake yeyote kutokamana na wazee au watoto au mji ndio anae tukanwa, wala si mafungamano tu… Fahamu!

## Kupenda Mji ni Maumbile ya Ubinadamu Wala si Tabia ya Kijahilia

**Na miongoni mwa kibaya zaidi ni katika yale yanayorushwa au kutupwa katika kuregesha maana ya kupenda mji ni kusema kuwa kupenda mji ni katika fikra za kijahilia au ni mawazo ya kijinga. Ni kama wanamaanisha neno lolote linalokusanya maana ya neno kupenda mji ni kitu kilicholeta vitendo au tabia za kijahilia au za kijinga. Uhakika umethubutu na tumejua kuwa kupenda mji ni jambo la maumbile na kuwa ni jambo lililoko katika tabia ya kila binadamu wakiwepo na manabii na wanavyuoni na wema licha na wasiokuwa wao. Basi asemae kuwa kupenda mji ni katika tabia za kijinga au kijahilia ni kama anawatuhumu wote hao kwa kule kulazimiana kwao na sifa hiyo ya kupenda mji na wala haliondoki hilo kwa neno kuwa sifa hiyo au tusi hilo lipo ati kwa kwa yule aliyejisalimisha kwa kupenda mji tu si kwa aliyepigana jihadi na akaacha kulifwata hilo la jihadi na sisi twasema kuwa watu waliobobea katika elimu na Imani wakiwemo manabii hakuna yeyote kati yao aweza kuwa na wazo hili la kijinga kama wanavyodai wao.**

## Ukoloni Iliweka Mipaka na Wala Haikuweka Mji

Wanadhania hawa wenye itikadi kali kuwa miji ya leo ni kutaka kugawanywa ukoloni katika ardhi za umma wa kiislamu.

Hii ni fikra punguani moja kwa namna nyengine kuwa haikuanzishwa mji na mkoloni na hata kugawanya na kuchorwa mipaka haikubadlishwa au kufanya upya mafungamano au kuleta uwiano baina ya watu na mji na hata kama ikileta athari juu ya harakati ya Muislamu na kugura kwake baina ya dola ya kiislamu na dola ya kiarabu.

Ama dola zingine na imarati na wilaya tukiangalia kwa upande wa kisiasa ni jambo la kitambo katika tarekhe za Waislamu. Ilianza dola kubwa kisha zikafarikiana dola ndogo ndogo. Kisha zikaungana na kutengana na hivyo hivyo. Na wala hakukuwa wakati wa mkoloni wala mkono wowote wa nje ule katika kuigawanya miji hiyo.

Na hapa twalitilia nguvu zaidi na kuwa hakuna upingamizi baina ya kuwa hizi miji zote ni zenye kuingia katika mipaka ya siasa moja kwa namna nyengine. Na mtu kujinasibisha kwa mji wake na kupatikana maana kufungamana nayo na kulazimiana nayo kuilinda na kuitumikia miji yake na watu wa mji wake haileti upingamizi kuwa hali yeyote na kujinasibisha na umma na uislamu wake.

## Msingi wa Kufahamu Ukazi wa Mji

### Ukazi

Linakusudiwa nayo haki na yanayopasa yanayofungamana juu ya ulimwengu wa kibinadamu kuwa yeye ni moja kati ya mji ambayo yanalingana ndani yake wote bila ya kubagua sawa awe juu ya misingi ya kidini au lugha au jamii au jinsia pia.

**Jambo ambalo kwamba laondosha au yatakikana waondosha utofauti wao na ikhtilafu wao katika kushirikiana na kusaidiana katika kujenga mji na kujinasibisha na kuhifadhi juu ya maisha wanaoshirikisha ndani yake.**

**Na hii ni kama desturi iliyodhihiri hivi karibuni. Ama kama kusudio na matangamano, ni kitu kipo juu ya ardhi tena tangu zama za Mtume (rehma na amani ziwe juu yake na jamaa zake) na pana hoja juu yake. Na ni katika makubaliano ya Madina kuwa "Mayahudi ni umma pamoja na Waumini. Wana dini yao na Waislamu wana dini yao. Watawala wao na nafsi zao ila atakaedhulumu na kutenda madhambi." Zingatia!**

# Natija ya Fahamu Gonjwa Kuwa Maana ya Mji na Ukazi

**Kuchukia Mji:**

Kwa hoja kuwa ni sababu ya kuwatenganisha Waislamu, na kuwa ni jambo linalopingana na kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na ni jambo linalokhalifiana na Sheria.

**Kukosa Kulazimiana na Kanuni au ya Lazima Katika Mji :**

Kwa hoja kuwa mji si kitu kinachotakiwa. Basi hana hamu ya kuujenga wala kuuimarisha!

**Kukosa Kuuhifadhi Juu ya Umoja wa Mji:**

Hawatilii manani. Badala kuliko kusaidia ili kupatikana mji wenye umoja wenye nguvu, yuaenda mbio katika kuubomoa na kuisamba ratisha ili ajengaye anayoyafikiria yeye kuwa ni mji!

**Utawala wa Dola au Mikusanyiko ya Kifikra Nyengine:**


Aona kuwa ni vyema zaidi kuongoza Waislamu.

# UFUPISHO:

1) Kupenda mji ni maumbile ya Kimola ambayo amemuumba nayo mwanadamu.
2) Kupenda mji ni jambo lililotolewa ishara na Qurani na ikabainishwa na hadithi na ikaja maisha ya wanavyuoni na wema wenye adabu na wengineo.
3) Mji ni kitu chenye maelezo na mkusanyiko uliopandamanishwa na kushikana kutokamana na ilaka na hisia wala haifai kuikata kabisa katika kusema, "ni mkusanyiko tu wa teko la mchanga."
4) Kupenda mji ni katika kumpenda Mola na Mtume wake wala hakuna pingamizi baina yao ila katika akili ya wenye itikadi kali. Kupenda mji ni sawa na kupenda family na jamaa na wala si katika maneno ya kijahilia kijinga katika lolote na wala si mbadala na undugu wa Kiislamu. Bali ni mzunguko wenye kulingana usio pingana.
5) Ukazi una haki zake alithibitisha Mtume (rehma na amani ziwe juu yake) kama ilivyo katika ahadi ya Madina iliyonawiri.
6) Kusema kuwa kupenda mji yapingana na kumpenda Mwenyezi Mungu na ya uhufu Uislamu iwe hatari yake kubwa juu ya mtu kwa yale anayoyazungumzwa kutokamana na kuweka mbali fikra na kuleta fujo baina ya maumbile na kutwii hizi fikra zinazo nasibishwa kwa uzushi kwa Uislamu. Fikra hiyo ina hatari juu ya mji wake hajinasibishi nayo, na wala hawi na pupa na mji wake. Bali hataki hata maendeleo na mji kun'gaa wa la hawla wa la quwwata illa Billahil-Adhim.

Na mwisho...
kupenda mji na kuhifadhi na kujinasibisha nayo ndio hatua ya mwanzo ya kujenga umma jamii, lau wangelifahamu...

# Kulingana Wala Si Kupingana





DAR AL FAQIH

مؤسسة طابة
Tabah Foundation
www.tabahfoundation.org

www.sanad.network

facebook.com/sanadnetwork
twitter: @sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork